



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

**MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2022 NA
MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2022.**

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2022.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo Kusini (St. Helena na Mascarene) iliimarika wakati ile iliyopo Kaskazini (Azore na Siberia) iliendelea kudhohofika. Hali hii iliendelea kusababisha kusukumwa kwa ukanda mvua (ITCZ) kuelekea Kaskazini zaidi mwa nchi yetu huku ikiambatana na kuimarike kwa tabaka mgandamizo mkubwa wa hewa maeneo ya mwambao wa pwani yote ya nchi. Katika eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola), joto la bahari lilikuwa la juu kidogo ya wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusukuma upopo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea kwenye maeneo ya Magharibi mwa nchi yetu.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA

Kwa ujumla, viashiria tajwa hapo juu viliendelea kusababisha vipindi vyta mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria. Aidha, maeneo ya ukanda wa pwani ya Kaskazini yalikua na vipindi vichache vyta mvua nyepesi ziliambatana na vipindi vifupi vyta upopo mkali. Hata hivyo, maeneo mengine yaliyosalia yalikua makavu kwa ujumla yakiambatana na vipindi virefu vyta juu.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2022

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2022

Katika dekadi hii tunatarajia migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) kuendelea kuimarike wakati ile iliyopo katika kizio cha kaskazini (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhooftika zaidi. Hali hii itaendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusogea kuelekea Kaskazini zaidi mwa nchi ikiambatana na kuimarike kwa tabaka la mgandamizo mkubwa wa hewa katika maeneo mengi ya nchi yetu. Joto la bahari katika eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani na hivyo

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

kuwa na mchango mdogo katika kusababisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea Magharibi mwa nchi yetu. Joto la bahari katika upande wa Magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani wakati upande wa Mashariki kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani. Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango mdogo katika kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya Mashariki mwa nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2022.

Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo za radi.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache vinatarajiwa.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vichache vya mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache vinatarajiwa.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa kipindi kirefu isipokuwa vipindi vichache vya mvua nyepesi vinatarajiwa hususani katika nusu ya kwanza ya dekadi.

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz